Mariam H. Maganga,
C/o RAAWU – Kanda ya
Mashariki,
S.L.P. 16421
DAR ES SALAAM

Mkurugenzi wa Mashtaka,
Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka,
Wizara ya Katiba na Sheria,
S.L.P.
DAR ES SALAAM.

21/08/2011

Ndg Mkurugenzi wa Mashtaka,

YAH: MALALAMIKO YA KUACHISHWA KAZI KWA KUTUHUMIWA NIMEPELEKA RIPOTI IKULU ZA UFISADI WA CHUO CHA TAIFA CHA USAFIRISHAJI NA KUREKODIWA SAUTI

Ndg Mkurugenzi, Mimi Mariam H. Maganga Elimu yangu ni ya Sekondari niliajiriwa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji mnamo tarehe 7/9/1990 kama Katibu Muhtasi Daraja la III na Kamati Ajiri kutoka Utumishi wa Umma Magogoni. Nimeachishwa Kazi 6/10/2008 nikiwa Katibu Muhtasi Daraja I, ndio mwanzo nimemaliza masomo ya (Diploma in Secretarial Duties) nimefaulu na nimewakilisha Cheti, sijapandishwa Cheo ndio ninaachishwa kazi kwa Tuhuma hizo hapo juu.

Mnamo tarehe 21/12/2007 Mkuu wa Chuo Mstaafu Ndg Ahad Rashid aliitisha Kikao ofisini kwake saa nane mchana baina ya mimi, M/Kiti RAAWU, Katbu RAAWU, Mkurugezi wa Utawala na Fedha, Mkurugenzi wa Taaluma na Meneja wa Utawala. Katika barua ya wito haikuonyesha agenda yoyote ya kikao hicho ili kukwepa ushahidi watakapo ni hoji kuhusu Tuhuma hizo. Na hata Wajumbe wengine wa RAAWU walishangaa hawakuitwa kwenywe kikao ikabidi wafosi kuingia.

Ndg Mkurugenzi, ndani ya kikao Ndg Ahad Rashid alinitupia Tuhuma nzito ambazo si za kawaida za kwenda ~~na~~ Ikulu, na Kurekodiwa. Ikulu ni mahali patakatifu na penye uaminifu, mnamo tarehe 26/09/2008 Kaim Mkuu wa Chuo Ndg Elifadhil Mgonja ndio anaripoti kutoka safarini Israel nikiwa ofisini kwake kufuatilia barua niliyoshindwa kuisaini 25/09/2008 kwasababu ya mazingira ya kutatanisha naye nilitupia Tuhuma hizo hizo za Ikulu kwa mara ya pili, na alisisitiza sisi ni Waalim tukifukuzwa tutapata kazi je wewe tukikufukuza utapata wapi kazi?

Tarehe 6/10/2008 nikiwa likizo ya mitihani ndani ya chumba cha mitihani nikapigiwa simu na Mama Judith Kiluswa nikachukue barua nilipofika nikakuta nimeachishwa kazi. Kwasababu nimemwagiwa ugali nami nikaamua kumwaga mboga, nilienda Takukuru na kwa Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali wakanisikiliza kilio changu na kuingia Chuo Cha Taifa Cha Usafirishaji kufanya uchunguzi wakakuta ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma na file la NIT liko kwako Ndg Mkurugenzi.

Ninachoomba file liharakishwe liende Mahakamani sheria ichukuwe mkondo wake mimi nimeadhirika sana na Tuhuma hizi na nikaamua kufanya kweli ubadhirifu upo wapelekwe Mahakamani. Na kama wanalindwa nami nirudishwe kazini.

Nitashukuru Ndg Mkurugenzi, file la NIT likifanyiwa kazi si UDA pekee kwenywe ubadhirifu hata Chuo Cha Taifa Cha Usafirishaji kina ubadhirifu mpaka kife kabisa ndio hatua zichukuliwe? Mbona Wabunge walioibua sakata la UDA hawa kuachishwa kazi? .

MARIAM H. MAGANGA – 0717 427210
MLALAMIKAJI

Nakala: 1. Waziri Mkuu
2. Waziri wa Uchukuzi
3. Katibu Naib RAAWU – Makao Makuu
4. RAAWU – Kanda ya Mashariki

Mariam H. Maganga,
C/o RAAWU – Kanda ya
Mashariki,
S.L.P. 16421
DAR ES SALAAM

Wah. Kamati ya Bunge la Miundo Mbinu, 04/08/2011
Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
S.L.P.
DODOMA.

Aione: Mh. Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Miundo Mbinu,

YAH: MALALAMIKO YA KUACHISHWA KAZI KWA KUTUHUMIWA NIMEPELEKA RIPOTI IKULU ZA UFISADI UNAOFANYWA NA CHUO CHA TAIFA CHA USAFIRISHAJI AMBAYO NI TAASISI YA MIUNDO MBINU

Ndg Wah. Mimi Mariam H. Maganga Elimu yangu ni ya Sekondari niliajiriwa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji mnamo tarehe 7/9/1990 kama Katibu Muhtasi Daraja la III na Kamati Ajiri kutoka Utumishi wa Umma Magogoni. Nimeachishwa Kazi 6/10/2008 nikiwa Katibu Muhtasi Daraja I, ndio mwanzo nimemaliza masomo ya (Diploma in Secretarial Duties) nimefaulu na nimewakilisha Cheti, sijapandishwa Cheo ndio ninaachishwa kazi.

Ndg Wah. Bunge, Mnamo 03/08/2011 nilikuwa makini kusikiliza Kikao cha Bunge cha 39 kilichohusu Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi ambayo ilikuwa Wizara yangu. Nilisikitika sana kusikia sakata la UDA pekee linalohusu ufisadi bila kugusia Chuo Cha Taifa Cha Usafirishaji ambacho kina lalamikiwa mda mrefu kwa ufisadi uliyokidhiri mpaka hali ya Chuo imekuwa mbaya, au nacho kinangojewa mpaka kife kabisa ndio hatua zichukukuliwe? Sasa ninaleta malalamiko haya kwenu Ndg Wah. Kuna kifungu gani cha sheria kwa mtu anaye fichua maovu kuachishwa kazi? Mimi nilipo achishwa kazi niliamua kufanya kweli na ukweli ukabainika ya kwamba kuna ubadhirifu mkubwa wa mamilioni ya pesa katika Chuo Cha Usafirishaji ambao ni mradi wa viongozi si UDA pekee.

Ndg Wah. Bunge, ubadhirifu huu nimeushughulikia mwenyewe na kuhakikisha file limefika kwa DPP na Mahakamani kwaajili ya sheria ichukuwe mkondo wake kama mimi nilivyowajibishwa, na kama hawakuchukuliwa hatua zozote nirudishwe kazini na kulipwa haki zangu zote. Kwasababu wahusika inavyoonyesha wanalindwa lakini tukumbuke kauli ya Mh. Rais aliyoitoa mwaka 2007 Nanukuu: Pale unapo ona mahali kuna ubadhirifu wa pesa toa taarifa. Leo hii mimi nina achishwa kazi kwa kuokoa pesa za Umma ambazo ni Kodi ya wananchi.

Ninaiomba Serikali na Bunge lako Tukufu ilishindikize File lililopo kwa DPP liende Mahakamani na wahusika wasimamishwe kama Ndg Jairo kwani kazi yote nimeshaimaliza, na liingilie kati suala langu kwani limechangia kukosa haki zangu na nyingine kudhulumiwa, na hata kufanya wafanyakazi mahali popote wanapoona maovu yanatendeka watashindwa kutoa taarifa. Na pia nimeshaadhirika kisaikolojia baada ya kunyimwa vitendea kazi kwa makusudi na kuanguka ni kavunjika chini ya uti wa mgongo na kupata kilema cha maisha kwasababu nimefichua maovu, Ndg Wah. Bunge tangu niachishwe kazi nimetumia pesa nyingi kwaajili ya matibabu na bado ninahitaji matibabu sina pesa.

Ni matumaini suala hili litashughulikiwa kama UDA wanavyoshughulikiwa.

Ahsante Wah. Wote katika Bunge letu Tukufu

MARIAM H. MAGANGA
NI MIMI MLALAMIKAJI MWENYE UCHUNGU NA CHUO

Ninaambatanisha vidokezo

N:B: Mnamo mwaka 2000 had 2004 kulikuwa na Mkuu wa Chuo Ndg Saad Fungafunga alituhumiwa na tuhuma kama hizi japokua hazikuwa na vielelezo na alitolewa kwenye Gazeti. Mara moja aliondolewa hawa waliopo kuna agenda gani?

Mariam H. Maganga,
C/o RAAWU – Kanda ya
Mashariki,
S.L.P. 16421,
DAR ES SALAAM.

Mh. Rais (Mrisho Jakaya Kikwete,
Ofisi ya Rais,
S.L.P.
DAR ES SALAAM.

18/08/2011

Ndg Mh. Rais,

YAH: KUACHISHWA KAZI KWA KUTUHUMIWA NIMEPELEKA RIPOTI IKULU ZA UFISADI WA CHUO CHA TAIFA CHA USAFIRISHAJI (NIT) NA SAUTI KUREEKODIWA

Ndg Mh. Rais, niliajiriwa tarehe 7/9/1990 na Chuo cha Usafirishaji pamoja na Kamati Ajiri kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma (Magogoni). Nimeachishwa Kazi tarehe 6/10/2008 nikiwa likizo nikishiriki mitihani ya kidato cha nne nilipopata barua ya kuachishwa nilishindwa kufanya mitihani nili changanyikiwa Mh. Rais, gharama zote nilizotumia zilipotea.

Ndg Mh. Rais, nilipoifungua barua nilichokiona ndani nilishangaa kasababu sijakaliwa kikao na kuulizwa hizo Tuhuma zilizokuwa ndani ya barua angalau nikajitetea ukweli ukapatikana sivyo. Na hata mtu akiuwa ana pewa nafasi ya kujieleza na kujitetea.

Chazo:
Ndg Mh. Rais, mwaka 2006-2007 nilikuwa masomoni Chuo cha Utumishi wa Umma nikichukuwa masomo ya (Diploma in Secretarial Duties). Nadhani kama utakumbuka ulipokuja kufungua rasmi Chuo chetu tulikujulisha mengi juu ya waajiri na wakuu wa Idara wanavyotunyanyasa hasa sisi makatibu muhtasi nilipomaliza masomo nilifaulu na kuripoti kazini nilishangaa kukuta mazigira yamebadilika kuliajiriwa makatibu muhtasi wawili, mmoja amewekwa kwenywe Idara yangu mimi nikaambiwa kwa mdomo na (supervisor) nenda ukafanye kazi Maktaba. Ambapo si jambo la kawaida mtu anaporipoti unajibiwa kwa barua. Nimeachishwa kazi sijapandishwa Cheo na mshahara kwasababu nimewakilisha Cheti.

Ndg Mh. Rais, baada ya kuchunguza katika makatibu muhtasi wale miongoni ni jamaa wa Mkurugenzi na ameajiriwa na (provision) si (transcript) (provision) inakujulisha masomo uliyosoma na mengine uliyofeli hupati cheti, (transcript) inakujulisha umefaulu masomo yote lakini unasubiri Cheti. Taratibu na kanuni mwajiri ana haki ya kuajiri na (transcript) sio (provision). Wakati naripoti

maktaba nilikuta hakuna vitendea kazi nikawa ninafanyakazi katika mazingira magumu mno, mazingira hayo ni pamoja na kutoa photocopy vitabu vya wanafunzi na hairuhusiwi mtu yoyote kushika photocopy ukimaliza hapo unapiga kadi kwenywe (typewriter) na kuingiza data kwenywe computer. Computer ikawa ina ubovu ukichelewa kusevu kazi inapotea. Idara nyingi zimepangiwa makatibu hawana sifa za kazi na wengine ni vibarua.

Ndg Mh. Rais, niliandika barua kwa Mkuu wa Chuo na kumjulisha hali ya vitendea kazi zaidi ya mara tatu sikujibiwa kwa bahati mbaya nilianguka na kuvunjika chini ya uti wa mgongo, wakati ninaendelea na matibabu niliandika barua na kambatanisha na X- ray yangu pia sikujibiwa bado niliendelea kukalia kiti kibovu kumbe nia na madhumuni niache kazi mimi mwenywe. Kwa bahati nzuri nikachaguliwa mjumbe wa Halmashari (RAAWU) nikawa ninaingia katika vikao vya bajeti ya Chuo nikiingia kwenywe kikao kitu cha kwanza na kumbushia vitendea kazi kwasababu nilikuwa siwezi kukaa vizuri kwenywe kiti kwa ajili ya maumivu ninayoyapata, lakini nikiongea na Mkuu wa Chuo Mkurugenzi wa Utawala na Fedha Ndg Eliezer Msonge anajibu yeye pesa hakuna wajumbe wenzangu wakanishauri nisikate tamaa andika (Requestion Purchasing) niliandika hadi kufikia (Voucher) ilipofika kwa Mkurugenzi aliiweka (Pending). Alinifanyia hivi kwa makusudi kwani wakati huo vifaa vingi vilinunuliwa na kwasababu huko nyuma aliwahi kunidhalilisha na matusi makubwa ya nguoni na kuniomba msamaha. Ndio tabia yake ya kuwatukana wafanyakazi na kuwafokea kama mbwa.

Ndg Mh. Rais, nilipoona mateso na manyanyaso yanazidi nikakimbilia Wizarani (Wizara ya Miundo Mbinu) nikamuona Katibu Mkuu Ndg Bukuku nikamwelezea yote niliyotendewa, na Ndg Bukuku alimwita Katibu msaidizi Ndg Chambo naye aje asikilize. Katibu Mkuu alianza kuunda Tume ya kushughulikia suala langu kwa bahati mbaya ukamteua kwenda Benki Kuu. Katibu msaidizi Ndg Chambo hakulishughulikia suala langu, mnamo tarehe 21/12/2007 nikapata barua ya wito ofisi ya Mkuu wa Chuo barua ile haina agenda na baadhi ya wajumbe walishangaa nilipoingia kwenywe kikao nikashutumiwa mimi nimekwenda Ikulu kutoa taarifa za ufisadi wa Chuo na Kurekodiwa Sauti na hata nikipeleka nyaraka yoyote inatiwa ndani ya dustbin.

Ndg Mh. Rais, baada ya kusikia tuhuma zile nilishindwa kujibu ila niliomba barua zangu nilizoomba vitendea kazi nijibiwe bado napata maumivu hasa ninapo inama na kutoa photocopy, niliposhindikana tarehe 23/06/2008 kwenywe Bodi ya Chuo mimi ni mtu mdogo si ajiriwi na Bodi. Niliitwa kwa mdomo ofisi ya Mkuu wa Chuo kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 6: 25 nikaletewa barua nisaini ndiyo niingie kwenywe kikao nilishindwa kusaini kwasababu ni kitu cha kushtukizwa niliitwa niingie nikakuta wajumbe wa Bodi wote wana makablasha ambayo yana tuhuma zangu. Mimi sikupewa kablasha hilo, nikasomewa tuhuma za kupeleka taarifa Ikulu pamoja na kutuhumiwa mwizi nimeiba flash disk ya Chuo, Mkurugenzi alindelea kunichafulia jina.

Ndg Mh. Rais, nilijieleza kwa wajumbe wa Bodi wakaridhika hasa hili la flash disk kwasababu nilikuwa na ushahidi niliazima kwa mwalimu na mwalimu alipobainika alipewa Onyo nikahoji kwa wajumbe ni kwanini niitwe mwizi? Tuhuma za Ikulu hawakua na ushahidi wowote. Nami nikaelezea wajumbe manyanyaso anayonipa Mkurugenzi na matusi anayonitukana pamoja na vitisho vya kuniachisha Kazi nikawaonyesha X- ray yangu wajumbe wa Bodi ndipo nikanunuliwa kiti na meza ya ofisi. Lakini hakuna Mhutasari wowote nilioupata wa kikao kuhusu mhusika wamemchukulia hatua gani mpaka Mkuu wa Chuo Ahad Rashid akastaafu.

Ndg Mh. Rais, tarehe 1/09/2008 - 26/09/2008 Mkuu wa Chuo anayekaim Ndg Elifadhil Mgonja alikuwa safarini Israel safari ya Hijja, Ndg Eliezer Msonge alkaim Mkuu wa Chuo akawa ameshika vyeo 3, mimi sina mahali pakumbilia akanitafutia tuhuma za kuninyima likizo yangu ya mwaka na kukataa kupokea mawasiliano ili mradi atafute chanzo cha kunitoa kazini. Tarehe 29/09/2008 niliitwa tena kwenye kikao cha Bodi barua ya wito nilipewa mapema tarehe 26/09/2008 nije na mtetezi wangu tulipoingia kwenywe kikao nikakuta wajumbe walewale walioshindwa kutatua matatizo yangu na kumchukulia hatua mhusika kwasababu ushahidi wa matusi aliyonitukana ulikuwepo nilitukanwa mbele ya Katibu wa (RAAWU) Mama Hilda Mteki. Wajumbe waliniuliza kuhusu mawasiliano na likizo nikajieleza wakaridhika, lakini hakuna Mhutasari wa kikao sikupewa hadi nimeachishwa kazi.

Ndg Mh. Rais, nikiwa katika likizo ya mitihani ambayo nilipitishiwa likizo hiyo. Ndani ya chumba cha mitihani nikapigiwa simu na Boss wangu kujulishwa barua nilipokwenda kuchukua nikakuta nimeachishwa kazi. Ni kaenda (RAAWU) kwa Katibu akasema bado tunakutambua ni mfanyakazi wetu. Sisi hatukushirikishwa wala huna Onyo hata moja na barua uliyoachishwa kazi haina nakala RAAWU – kwa taarifa.

Ndg Mh. Rais, Nilienda RAAWU – Kanda kwa Mama Theresia Manamba alinishughulikia ndiye mwakilishi wangu CMA. Chuo kilileta mawakili wawili mwajiri hakuja na alitakiwa aje mwenyewe ndiyo maana ya (mediation) na najua sababu zilizomfanya asije kwasababu maelezo yangu yalikuwa ya kweli wakili wa Chuo alikubali. Msuluhishi akasema nirudishwe kazini wakili akatoa kablasha na kudai tuhuma zangu, Msuluhishi alipozisoma aliona tuhuma si za kweli, wakili aliniomba niombe msamaha ikashindikana.

Ndg Mh. Rais, katika Ziara yako ya Wizara ya Ajira na Kazi Mh. Waziri alitoa maelezo kesi nyingi zinamalizika kwa njia ya suluhu kati ya mwajiri na mwajiriwa si kweli waajiri huwa hawaji wanafanya hivi kuona kwamba wao ndiyo wenywe makosa, na wanatoa mianya ya rushwa kupitia kwa mawakili na waamuzi kwa

sababu wamezoana mara kwa mara wanaonana njia hii ni rahisi mwajiriwa kukandamaizwa na kuandikiwa vitu vya uongo ndani ya ushauri na uamuzi. Na kwa sababu hakuna (rekoda kwenywe vyumba) ni rahisi kubambikiwa maneno ya uongo na kujulikana mwajiri ndiyo mwenywe ukweli.

Ndg Mh. Rais, nilipoachishwa kazi niliamua kwenda Takukuru na kwa Mkaguzi wa Mahesabu ya Serikali waliingia pale Chuoni walikamata ubadhirifu wa mamilioni ya pesa file lao liko a DPP na jingine Mahakama ya Kinondoni Na. URP/2834/2009 Mh. Rusema. Ndg Mh. Rais, nimeokoa pesa nyingi ambazo ni kodi za wananchi siyo UDA pekee.

Ninachoomba Mh. Rais, nirudishwe kazini mimi nimeshaadhirika na ulemavu huu ambao uko sehemu nyeti ambao ni muhimili mkubwa katika kiungo cha binaadamu nami nimfanyakazi wa mda mrefu miaka 20 nina umri wa miaka 50 ninasubiri (pension). Kesi yangu iligubikwa na mchezo mchafu ili nikandamizwe nikose haki. Mama Theresia Manamba wa RAAWU ni shahidi kwa yote aliyoyaona CMA.

Ndg Mh. Rais, tangu nimeachishwa kazi nilikwenda Wizarani, Wizara haikunishughulikia, nimeandika barua kwa Mh. Waziri Mkuu bado sijajibiwa, nimeandika Wizara ya Kazi zaidi ya mara mbili kuhusu maonevu sijajibiwa, ndiyo sababu nikaamua kukuandikia Mh. Rais. Kwasababu nimefuata ngazi hadi ngazi lakini hakuna mafanikio ya kutendewa haki nami ninateseka na watoto.

Mariam H. Maganga
Mlalamikaji

WIZI UNAOTUMIKA NIT KWA KUIBIA SERIKALI NA MATUMIZI MABAYA YA FEDHA BAADA YA KUACHISWA KAZI KWA KUHISIWA NINAKWENDA IKULU KUTOA TAARIA. NDIPO NILIPOAMUA KWENDA KWA MKAGUZI MKUU WA MAHESABU YA SERIKALI NA TAKUKURU KUTOA RIPOTI HIZI.

1. **Mwaka 2003 mwezi wa 7 Ndg Msonge aliajiriwa, kabla hajadhibitishwa kazini alikopeshwa gari aina ya PRADO. Tarehe 2/11/2004 jumla ya shs 1,136,500/= ziliombwa kwaajili ya kununulia matairi ya gari lake T390 ABH kwa kisingizio ilikuwa inatumika kwa ajili ya kazi za chuo, lakini sikweli. Kwa kumtumia James Mosha (Transporter Officer), na hali wakijua wote kwa pamoja wamefanya makosa, bila kupitia kitengo cha Ununuzi (Stoo) na kutumia GRN. Kama taratibu za vifaa vyote vya chuo, na kuandika risiti ya mkono ili itambulike ni risiti halali, matairi ya zamani haya kurudishwa stoo. Matairi hayawezi kuisha ndani mwaka 1. (huu ni wizi)**

2. **Mkurugenzi (Eliezer Msonge) kuagiza watu wa Uhasibu wamnunulie simu za mkononi bila kufuata taratibu za manunuzi kwa kupitia kitengo cha stoo kama kweli ni haki yake. Na hali akijua analolifanya ni kosa, mpaka sasa ameshanunuliwa simu 3 bila kurudisha zile zilizo haribika. (Haya nimatumizi mabaya ya fedha za umma)**
3. **Tarehe 14/9/2006 NIT ilitoa Zabuni kwa Cariton Trading Co. ya kununua vifaa vya Karakana vyenye thamani ya shs 29,000,000/= pesa ambazo zimelipwa na TEA kwaajili ya NIT, lakini cha kushangaza NIT bila kuzingatia taratibu za mkataba wakawalipa Cariton (advance) ya shs 10,000,000/= ili ziwezeshe kununulia vifaa. Bado aliendelea na mtindo huohuo wakuchukua pesa kwa kutumia kisingizio cha TEA aliidhinisha shs. 4,000,000/= kwaajili ya ufuatiliaji vifaa tulivyo pata msaada kutoka TEA. Mkataba ulioandikwa ni wa Uongoa kutoa 10,000,000/= wakati pesa zimeshalipwa wamefanya ubadhirifu na toka lini vifaa vya Msaada vikafuatiliwa? (huu ni wizi),**

4. **Ndg Msonge alishirikiana na mnunuzi wa vifaa vya Chuo Ndg Mwajuma ambaye ameacha kazi na kukimbilia TRA, kula njama kwa kununua (Anti virus za computer) za Chuo zenye thamani ya shs 6,080,600/= vile vifaa havijafika hadi leo pesa hizi zimeliwa**
5. **Mwaka 2005, Ndg Msonge akishirikiana na Mwajuma kupandisha bei ya vifaa vya Chuo kwa mfano Vitasa vya milango Union shs 10,000/= wanaandika shs 25,000/= kitasa kimoja, vitasa hivyo vilikuwa kwaajili ya milango yote ya Mabweni Flashs Disk ni sha 30,000/= hadi 70,000/= lakini wanaandika shs 150,000/= flash disk moja, na kuagiza Tonner feki za printer kwa kuweka bei za Tonner Original kuanzia za photocopy hadi za printer na kuuwa printer na photocopy kutengenezwa mara kwa mara. Ndg Amos Nsanganzelu aliyetoa ushahidi katika kesi hii (Internal Auditor) aligundua vyote hivyo wakati anakabidhiwa ofisi lakini alizibwa mdomo kwa kununuliwa gari. Baadaye aliacha kazi iliasipate lawama baada ya kusikia wakaguzi wahesabu za Sarikali wanaingia NIT**

6. **Mkurugenzi Ndg Msonge na wenzake wameleta mafundi wa mitaani kujenga Jengo la Dispensary kwa gharama ndogo na kuandika mamilioni ya pesa, mafundi hao hawakuyamaliza majengo hayo ikabidi wa watumie mafundi wa hapa Chuoni wafanye (finishing) na kuwalipa posho ndogo. Majengo mabovu yananyufa kibao (huu ni wizi)**

7. Mwaka 2004 waliweka bajeti ya kukarabati Madarasa, viti na meza lakini hali ya madarasa ni ya kusikitisha ni mbaya mmno, ukizingatia Chuo kikubwa kama hiki cha Kimataifa ni aibu kwa Serikali pesa zote wanakula mafisadi, kila baada ya miezi 6 kufanyia (service air condition) (wizi mtupu).
8. Magari ya kufundishia wanafunzi wa kozi za Udereva SCANIA yalikuwa yana andikiwa kujazwa mafuta na hali ni mabovu wakishirikiana na (James Mosha) yameuzwa mwaka 2006 wafanyakazi hatukuziona pesa kwa taarifa.
9. Ndg Msonge alimteuwa karani ambaye hana sifa (PGS 3) mshahara wake. Debora Peter kuwa Mkuu wa manunuzi ili amburuze kwa kile anacho kitaka kwasababu hana anachokijua kwa kununua thamani za Chuo kwa bei za juu pamoja na Bus bovu lilitumia shs. m. 230. wakishirikiana na James Mosha. Na huyo binti kununuliwa gari aina ya Starlet na kumiliki Stationary. Wakati huo wenye sifa za CPA wapo kwa kazi za manunuzi na wanafahamu taratibu zote za kazi. Yeye kama Mkurugenzi wa Fedha ametumia makosa makubwa na ukiukaji wa maadili na taratibu za kazi, baada ya wafanyakazi kulalamika akamuondoa wakati wameshaiba pesa nyingi (wizi mtupu),
10. Ndg Msonge, Ahadi Rashid, Senzighe na Mgonja wote wakiwa madarakani wameufilisi mradi wa masomo ya jioni hadi wakaufunga kabisa (kilikuwa kituo kikubwa kwaajili ya Mitihani ya kidato cha 4 na kilikuwa kinaingiza mamilioni ya pesa). Pamoja na kutoa ajria.
11. Ndg Msonge aliandika sifa za Uongo katika Jedwali la Majina yaliyokwenda Hazina, pale Chuo kilipo panda Daraja na kujiingiza katika Orodha ya Waalimu na kujilipa mshahara wa M. 3 bila kuzingatia ajira yake inasema nini, kwahiyo hakufuata ufundishaji bali amefuata pesa.
12. Mwaka 2006 Msonge kujipangia sehemu za mbali kwaajili ya kusupavaizi wanafunzi wakati anajua hajawahi kuingia darasani, anaenda kumsupavaizi nani? (wizi wa maandishi)
13. Msonge anapenda kusaini pesa wakati ameandikiwa barua ya Kukaim, Mkuu wa Chuo akienda Bungeni. Miaka yote ya nyuma anayekwenda Bungeni ni Mkuu wa Chuo tu lakin hii sasa wanakwenda watu 3 nakujilipa mamilion ya pesa. (matumizi mabaya ya fedha za Umma)
14. Kila mwaka watu wa Uhasibu wanapofunga mahesabu wanalipana posho ya mamilioni ya fedha, zaidi ya mishahara yao kuanzia Mkurugenzi hadi Sekretari wao. (Matumizi mabaya ya fedha za umma)
15. Mradi wa Kozi za Madereva unaingiza mamilioni ya pesa lakini maendeleo ya Chuo yanadidimia kwasababu ya Ufisadi unaofanyika kwasababu pesa hizi hazina usimamizi wa Serikali, na Maoditor wanaokuja kila mwaka kufanya mahesabu huwa wanapewa kitu kidogo ili kuficha madhambi yanayofanyika
16. Mwaka 2007 chuo kilipata kazi za Consultancy ya kuhesabu magari yenye thamamni ya shs m.80 waliwatumia wanafunzi kwa kazi hiyo na kuwalipa shs 15,000/= kwa siku kuanzia asubuhi saa 12.000 hadi saa 5.00 za usiku pamoja na chakula, Mkurugenzi alichukuwa mgao wa M. 4 wakati hakufanya kazi zozote. Ikiwepo na kazi ya kutengeneza Mitaala ya chuo pia anachukua pesa nyingi kuliko walioshiriki kazi hizo. (Matumizi mabaya ya fedha)
17. Mkurugenzi Msonge ndani ya miaka miwili amejenga nyumba ya Gorofa Kimara na anamiliki magari 3, Ng'ombe wa maziwa 20, amechimba kisima ambacho hakikauki maji na kutandikaa mabomba katika mto. Pesa zote hizi amezipata wapi kama siyo wizi wa mali ya Umma? Alipokuja kutoka TAZARA mafao yake alipata shs m.13 na amekuja na Landrover iliyochoka aliyouziwa na TAZARA nayo imetengenezwa kwa pesa za chuo.
18. Ndg Msonge nyumba yake iliyoko Temeke ameikarabati kwa pesa za Chuo pale Mwajuma anaponunua vifaa vya Zahanati ya Chuo kwaajili ya Ujenzi, na

19. Mkuu wa chuo mstaafu Ahadi Rashidi pamoja na Msonge walibadilisha enginer mpya kwenye magari yao zenye thamamni ya shs 4,780,000/= kila mmoja jumla walitumia shs 9,560,000/= barua hizo za manunuzi zilipelekwa usalama wa Taifa. Ahad Rashid baada ya kubadilisha enginer gari yake aliuza kwa thamani ya shs m.11. wakati yeye aliuziwa kwa shs m.8 mwaka 2003. Baada ya kuuza lakini bado alikuwa anachukua pesa za manunuzi ya mafuta kama walivyojipangia katika Bajeti zao za Ufisadi na huku wanatumia magari ya Chuo akiwemo na Ndg Mgonja, (matumizi mabaya ya pesa za serikali wakiwa madarakani) Ndg Rashid ana nyumba 6 moja ya Gorofa, anamiliki Bar kubwa Tabata ana magari 2 ya kutembelea na Hice 3.
20. Kozi za madereva zinazofanyika Mikoani, kulikuwa kuna posho zinazolipwa wafanyakazi kama motisha Ndg Msonge Mkurugenzi ameziondoa kwa kwafanyakazi wanakula wao na wenzake. Chuo kilipewa Msaada wa Magari mawili kwaajili ya Kozi za madereva kutoka Kahama Mining. Magari hayo hatujui yamekwenda wapi tume ambulia kuona makabidhiano ya funguo kwenye Kalenda za Chuo
21. Tarehe 4/9/2008 hadi 26/9/2008 Ndg Mgonja alikwenda Israeli safari ya kidini na kutumia mamilion ya pesa za Chuo, amejenga Gorofa Hotel ya kifahari Arusha. Na mara kwa mara safari za kwenda Arusha haziishi pamoja na Ndg Rashid kwa kutumia usafiri wa Ndege kujitengenezea mazingira ya kupata pesa. Wakati walipokuwa wakuu wa Idara safari zote wanatumia mabus kwaajili ya kubana matumizi kwa manufaa yake. Ndg Mgonja hana sifa za kuwa Mkuu wa Taalum Cheo hiki alipewa kwaajili ya ukabila na aliyekuwa Mkuu wa Chuo mstaafu Ahadi Rashidi
22. Kuwalipa masaa ya ziada jamaa zao wakiwa ni vibarua huku wakiwa masomo (Open University) anaondoka saa 9. lakini analipwa masaa ya ziada shs 300,000/= kwa mwezi hiyo kazi ameifanya saa ngapi? Wakati yuko chuo? Sasa hivi ameajiriwa kabisa (Upendo Urasa). Na wafanyakazi wengine wanafanya masaa ya ziada mwezi mzima lakini wanalipwa nusu mwezi. Wafanyakazi wamelalamika hadi wamechoka kwa kudhumiwa jasho lao
23. Wanajiwekea bajeti ya mamilioni ya fedha kwa mtu mmoja huku wakifuja mali ya umma, kama bajeti inavyo jieleza Uniform za wafanyakazi walipata mwaka 2008 tu baada ya kukaa kwa muda wa miaka 3, lakini kila mwaka wanaweka bajeti pamoja na (Repair maintenance) nyingi kama siyo wizi nini?
24. Ndg Msonge Mkurugenzi wa Utawala na fedha ametumia shs M. 400 kwajili ya Ujenzi wa (Foundation) tu, Jengo la Maktaba (Ufisadi mkubwa ulitumika katika Jengo hili) wa kukiuka taratibu za Manunuzi kwa makusudi na Kutoitangaza Tenda. Ikiwa Jengo la Maktaba ametumia M.400 Nyumba yake ya Gorofa moja imetumia mamilioni mangapi pamajo na ya Ndg Mgonja?

25. Ndg Eliezer Msonge Mkurugenzi wa Utawala na Fedha na Ahadi Rashidi Mkuu wa Chuo (Mstaafu) walimrubuni Msaidizi wa Mahesabu Ndg Kimbengele kukiibia Chuo M. 55 pesa za Kozi za Madereva wao wakiwa ndio wadhibiti wakuu wa pesa za Umma. Baada ya kuripotiwa kwa Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali alituma vijana wake kwenda kufanya ukaguzi ndio ukagundulika wizi huo. Waliendelea kumrubuni Ndg Kimbengele akubali kuwa yeye ndiye aliyekula pesa halafu wao watajuana na mpelelezi jinsi gani watapoteza ushahidi. Kitu cha kujiuliza ni kwanini kesi hii wameipeleka Polisi baada ya Wakaguzi kugundua? Taratibu na kanuni pesa zinapopelekwa Bank Mhasibu anajaza fomu kiasi cha pesa kinacho pelekwa Bank na

kuipeleka fomu ile kwa Mkurugenzi ili ahakikishe na kutia saini baada ya hapo inakwenda kwa Mkuu wa Chuo naye akahakikishe na kutia saini ndipo pesa zinapelekwa, Pesa hizi zimeliwa ndani ya mwaka mmoja ni kwanini wote wawili wasigundue mapema upotevu huu kama awakuhusika? Hata kama akikwepa sheria bado inambana kwa upotevu huo yeye ni Mkurugenzi wa Utawala na Fedha. Kazi yake ni nini kama si kudhibiti mali ya Umma? Alifaa awajibishwe kwa uzembe wa upotevu wa mali ya Umma.

26 Mkurugenzi Ndg Eliezer Msonge ana wafanyia fojari wahudumu kwa kuongea na Mkuu wa Chuo wa Mantap Bagamoyo (Maktaba) wakati akijua hawana sifa za kungilia ili awapokee. Kwasababu Chuo kiliajiri wafanyakazi wenye sifa za Maktaba na kuwalipa PGS 7 walifanyakazi miezi 2 wakaacha kutokana na mishahara midogo. Sasa anachokifanya Mkurugenzi huyu kwa hawa wahudumu aliyo wa peleka yeye. Kwenye Jedwali linalo kwenda Hazina anawandikia PGS 7. Mishahara anawalipa PGS 5. kwa hiyo wanaridhrika kwasababu wahudumu wanalipwa kuanzia P0S. Hili analolifanya anajua ni kosa kubwa na pia anadhorotesha hali ya Maktaba ya Chuo kutokua na watu wenye sifa stahili kwaajili ya manufaa yake binafsi. (huu ni wizi)

27 Mnamo 18/4/2008 tulipata barua kutoka RAAWU – Kanda ya Mashariki, ikitaka Orodha ya wafanyakazi na vyeo vya sasa walikataa kutoa kwasababu tutajua madhabi wanayoyafaya. Mimi nilikua mjumbe wa Halmashari ya RAAWU tulitakiwa tuhakiki zoezi hilo kasababu wanaandika majina hewa na vyeo vya uongo wanapopeleka hazina na pia anamtandao huko hazina kwa kumpa ajira Ndg wa Bwana Fedha ili kujenga uhusiano mzuri.

28 Ndg Msonge Mkurugenzi anawajiri jamaa zake wasio na sifa za Taaluma baada ya miezi kadhaa anawapeleka kusomea Taaluma kwa pesa za Chuo.

Namabatanisha Vipande vya Gazeti vilivyoelezea Ufisadi huo lakini kitu cha kushangaza watu hawa bado wapo. Mpaka Wanafunzi wakaamua kuwafungia Ofisi kuishindikiza Serikali kuwaajibisha hadi leo wapo. Wizi wao ni wakujiamini kwasababu wanalindwa kwani barua ya Ajira ya Mkurugenzi Refaree wake Ni Katibu MKuu Kiongozi Ofisi ya Rais Philemon Luhanjo na Katibu MKuu wa BAKWATA Ndg Hassan Luambano.